

TAARIFA KWA UMMA

UTOAJI WA LESENI KWA MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA, DODOMA (DUWASA)

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Bw. Haruna Masebu anapenda kuwataarifu wananchi wote kuwa tarehe 25 Mei 2007 EWURA itatoa leseni ya kwanza katika sekta ya maji kwa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka, Dodoma (DUWASA).

Tukio hilo litafanyika katika hoteli ya Protea (CourtYard) eneo la 'sea view', jijini Dar es Salaam kuanzia saa nne asubuhi. Mgeni rasmi atakuwa kuwa Waziri wa Maji Mhe. Dr. Shukuru J. Kawambwa (Mb.).

EWURA ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji inayoundwa kwa mujibu wa Sheria ya EWURA Sura ya 414. Sheria hiyo inaipa EWURA mamlaka ya kutoa leseni kwa Mamlaka zote za majisafi na majitaka hapa nchini. Pamoja na sekta ya Maji, EWURA pia inadhibiti utoaji wa huduma katika sekta za nishati zikiwemo umeme, mafuta ya petroli na gesi asilia.